



Tunajenga Maisha Yako  
ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

LA MTANDAONI | TOLEO LA OKTOBA 2021

## NSSF ILIVYOADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA



Tunajenga Maisha Yako  
ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

[www.nssf.or.tz](http://www.nssf.or.tz)

Simu Bure 0800116773  
[customercare@nssf.or.tz](mailto:customercare@nssf.or.tz)

@NssfTanzania





## KISHINDO CHA NSSF WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA “NGUVU YA HUDUMA”

### Na MWANDISHI WETU

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, aliungana na baadhi ya wafanyakazi kutoka Ofisi za Mfuko huo Ilala, Kinondoni, Temeke pamoja na vituo vilivyopo Dar es Salaam kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyoanza Oktoba 4 mpaka Oktoba 8, mwaka huu, ikiwa na kauli mbiu isemayo “NGUVU YA HUDUMA”

Maadhimisho hayo yalitanguliwa na matembezi ya amani ambapo Mkurugenzi Mkuu na wafanyakazi wote hao walikusanyika Makao Makuu ya Mfuko yaliyopo Jengo la Benjmini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza katika sherehe hizo ambazo zilihudhuriwa pia na Meneja Rasilimali Watu na Utawala, Ekwabi Mujungu pamoja na Meneja Huduma kwa Wanachama, Robert Kadege, Mshomba alisema katika kuwajali wateja na wanachama Bodi ya Wadhamini ya NSSF iliridhia kutoa msamaha kwa waajiri wote wenye malimbikizo ya michango na tozo zitokanazo na uchelewashaji wa michango.

“Katika hatua moja wapo ya kuonesha jinsi ambavyo NSSF tunawajali wateja na wanachama, Bodi ya Wadhamini iliridhia kutoa msamaha huo ambao ulianza rasmi tarehe 1 Oktoba, 2021 na unahusu waajiri wote wenye malimbikizo ya michango na tozo kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2021,” alisema.

Aidha, aliwasilitiza wafanyakazi umuhimu wa kuvali viatu vya wateja kwa kutoa huduma bora na stahiki kwa haraka kwani Mfuko una thamini wateja wake na kwa maana hiyo itaendelea kuwashumia wanachama kwa ubora na wakati ili kutimiza malengo na vipaumbele walivyojiweka.

# MATUKIO KATIKA PICHA NSSF DAR ES SALAAM



# MATUKIO KATIKA PICHA NSSF DAR ES SALAAM



### 3 KALI ZILIZOBAMBA

Kufuatia msamaha kwa waajiri wenyewe malimbikizo ya tozo zitokanazo na ucheleweshaji wa michango, hii ni motisha kubwa kwa waajiri wetu na tumeshapokea simu nyingi kutoka kwao ambapo wameonesha mwitikio mkubwa na tunatarajia tutakuwa tumeaadia kuondoa kero kwa wanachama wetu na inaonesha ni jinsi gani ambavyo tumejipanga katika wiki hii ambayo tunaimalizia.



Masha J. Mshomba  
**Mkurugenzi Mkuu NSSF**

Katika kutenda kazi kauli mbiu ya "Nguvu ya huduma" sisi NSSF tutahakikisha tunatumia mifumo ya kidigitali ili wanachama wetu waweze kupata huduma popote walipo pia tutahakikisha tunafanya kazi kwa ushirikiano huku tukitatua kero za wanachama kwa wakati.



Robert C. Kadege  
**Meneja Huduma kwa Wateja**

Tuwe na hofu ya Mungu kwani ukiwa na hofu ya Mungu utatoa huduma nzuri na huwezi kumtenda mabaya mteja wako na mimi kwangu wateja wa kwanza ni watumishi wenzangu, kwa msingi huo ukimuhudumia mteja wa ndani vizuri hata mteja wa nje utamuhudumia vizuri.



Ekwabi Mujungu  
**Meneja Rasilimali Watu na Utawala**



Tunajenga Maisha Yako  
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako  
ya Sasa na Baadaye

**NSSF**